**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU TABORA**

Anuani ya simu: “T.T.C.”
TABORA
Simu Na:
0262604939/0752416009
Fax: 0262604939
Email: taboratc@moe.go.tz.
**Unapojibu tafadhali taja:**

Chuo cha Ualimu Tabora,
S.L.P. 320,
TABORA
**TANZANIA**

**Kumb.Na.TBR/CCU/JI/VOL II/45** **02.06.2026**

……………………………………………………………………………………………………

**YAH: KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA MAALUMU YA UALIMU ELIMU YA MSINGI MASOMO YA SAYANSI/STASHAHADA YA UALIMU ELIMU MSINGI MASOMO YA SAYANSI NA HISABATI KATIKA CHUO CHA UALIMU TABORA MWAKA 2026/2027**

## 1.0: UTANGULIZI

Ninapenda kukuarifu kuwa umechaguliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kujiunga na Mafunzo ya **Stashahada Maalumu ya Ualimu wa shule ya Msingi masomo ya Sayansi/Stashahada ya ualimu elimu msingi masomo ya sayansi na hisabati** katika Chuo cha Ualimu Tabora. Chuo kinakupongeza Kwa nafasi hii. Tunategemea kuwa utatumia nafasi hii vizuri katika masomo yako. Hivyo, unatakiwa uwe na juhudi na moyo wa kujifunza darasani na nje ya darasa ili uweze kufaulu vizuri mafunzo yako.

**Kozi zinazotolewa katika chuo cha Ualimu Tabora ni kama ifuatavyo: -**

i) Stashahada Maalum ya Elimu ya Ualimu wa shule ya Msingi masomo ya Sayansi na Hisabati michepuo ya (PME, PCE, PBE, CBE, CME, na CSME), kozi hii ni kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha nne tu na wakafaulu masomo ya Sayansi na Hisabati.
ii) Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi masomo ya Sayansi na Hisabati, kozi hii ni kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha sita au waliomaliza mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti (Grade A)
iii) Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi kwa njia ya Masafa, kozi hii ni kwa wanafunzi waliomaliza mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti (Grade A) au walimu waliopo kazini wenye Astashahada ya ualimu.

## 2.0: MAHALI CHUO KILIPO

Chuo kipo Tabora mjini umbali wa kilometa moja **(1)** Magharibi mwa stesheni ya reli na kilometa moja na nusu **(1½)** Mashariki mwa kituo kikuu cha mabasi.

## 3.0: TAREHE YA KURIPOTI

Unatakiwa kuripoti Chuoni tarehe **17/08/2026**. Mwisho wa kuripoti kwa mwanachuo ni tarehe **31/08/2026.** Kwa wanachuo wa masafa watapaswa kusajiliwa rasmi na kuanza masomo yao kwa tarehe ya kuripoti iliyoainishwa hapo juu.

**TAHADHARI:** Mwanachuo akichelewa kuripoti/Kusajiliwa wiki mbili (SIKU 14) baada ya tarehe ya kuripoti chuo kupita hatapokelewa tena.

## 4.0: MUDA WA MAFUNZO

i) Muda wa mafunzo kwa kozi ya Stashahada **Maalum** ya Ualimu Elimu Msingi katika Masomo ya Sayansi na Hisabati ni **miaka mitatu**. Mwaka wa kwanza na wa pili mwanachuo atasoma masomo ya kidato cha tano na sita (A-Level) kisha atafanya mtihani wa taifa wa kidato cha sita (ACSEE). Mwaka wa tatu mwanachuo atajifunza masomo ya Ualimu na kufanya mtihani wa taifa wa ualimu. **Hivyo, kama mwanachuo alishafanya mtihani wa kidato cha sita kabla hatakiwi kusoma kozi hii.**

ii) Stashahada ya Ualimu Elimu Msingi ni **miaka miwili.** Kozi hii ni wale waliomaliza kidato cha sita au mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti (Astashahada ya ualimu elimu awali au msingi).

iii) Muda wa mafunzo ya ualimu kwa njia ya masafa ni miaka mitatu(3) hadi mine(4)

## 5.0: USAJILI

- Mwanachuo akifika chuoni, lazima aripoti kwa Mkuu wa idara ya udahili, mitihani na vyeti, ili apewe utaratibu wa namna ya kukamilisha usajili wake.

## 6.0: VYETI HALISI

- Fika na **CHETI HALISI (Original Certificate)** cha kumaliza Kidato cha nne na Cheti cha Kuzaliwa. Ikiwa cheti cha mwaka husika hakijatoka utatakiwa kuja na *result slip* ya mwaka husika.
- Pia, Uje na ***'Leaving Certificate'*** yako ya shule uliyomalizia kidato cha Nne isipokuwa kama ulikua mtahiniwa wa kujitegemea (private candidate). Kwa wanachuo wa masafa mwanachuo awasilishe cheti alichomalizia chuo cha Ualimu.

- **USIPOKUJA NA VYETI TAJWA HAPO JUU, HUTAPOKELEWA CHUONI. Tafadhali zingatia sana maelekezo hayo.**

## 7.0: BIMA YA AFYA NA T-SHIRT

- Kila mwanachuo anatakiwa kuja na kadi yake ya **bima ya afya** na kama hana atatakiwa kulipia fedha taslimu (cash) **Tsh. 50,400/=** kwa IT wa chuo kwa ajili ya kupata kadi y**a bima ya afya**, kwa kanuni na taratibu za chuo, **Bima ya afya ni lazima kwa kila mwanachuo.**
- Kila mwanachuo anatakiwa kupima afya yake katika hospitali za serikali zinazotambulika na kupigwa muhuri. Kwa mwanachuo mwenye changamoto kubwa ya afya tunashauri mara afikapo chuoni awe wazi kwa walezi na kuwa na uthibitisho wa daktari juu ya tatizo alilonalo sambamba na kuhakikisha dawa zake muhimu anazotumia zinafahamika kwa mlezi wa wanachuo na muuguzi wa chuo.
- Kila mwanachuo atatakiwa kulipia fedha taslimu (cash) **Tsh. 20,000/=** kwa ajili ya kupata T-shirt ya chuo na yenye nembo ya chuo. T-shirt hizo zinapatikana katika duka la chuo.

**N: B:** Kwa wanachuo wa bweni hakikisha siku ya kuripoti chuoni unakuja na fedha taslimu zilizoainishwa hapo juu (bima ya afya, T-shirt) ambazo jumla yake ni **Tsh. 70,400/=.** Mwanachuo hatasajiliwa kama hana fedha hiyo.

## 8.0: ADA YA CHUO

- Fedha ya **Ada** ya Chuo ni Tshs. **450,000/=** kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili yaani Tshs.**225,000/=** kwa kila muhula au unaweza kulipa kiasi chote Tshs. **450,000/=** kwa mwaka**.**
- **Ada** ya Chuo ilipwe kwa kutumia **"control number"** ambayo utapewa na Muhasibu wa Chuo au mkuu wa idara ya udahili, mitihani na vyeti mara ufikapo chuoni au kupiga simu kwa muhasibu au msajili ili utumiwe control number kupitia namba za simu zifuatazo:-
  **Mhasibu:** 0755 679 493
  **Msajili:** 0753 087 126

## 9.0: MICHANGO YA CHUO

Michango ya Chuo ni Tsh 150,000/= ambayo italipwa kupitia akaunti ya NMB yenye akaunti Namba **51001100030** na Jina la akaunti ni **"The Principal Tabora TC".** Utatakiwa kuwasilisha (stakabadhi) risiti ya malipo wakati wa kuripoti chuoni na ni **LAZIMA JINA LA MWANACHUO LIANDIKWE WAKATI WA MALIPO ILI LISOMEKE KWENYE BANK STATEMENT, tahasusi (combination) na mwaka wa masomo. Mchanganuo wa michango ya chuo ni kama ifuatavyo:-**

| S/N | MCHANGO | KIASI | MAONI |
|---|---|---|---|
| 1 | Serikali ya wanachuo | 5,000/= | Mwaka |
| 2 | Huduma ya kwanza | 10,000/= | Mwaka |
| 3 | Utunzaji wa Mazingira | 20,000/= | Mwaka |
| 4 | Godoro | 10,000/= | Mwaka |
| 5 | Usajili na Kitambulisho | 20,000/= | Miaka 3/miaka 2 |
| 6 | Michezo | 30,000/= | Mwaka |
| 7 | Ulinzi | 30,000/= | Mwaka |
| 8 | Ukarabati | 25,000/= | Mwaka |
|  | **JUMLA** | **150,000/=** |  |

### 9.2 MICHANGO KWA WANACHUO WANAOJIFUNZA KWA NJIA YA MASAFA

| S/N | MCHANGO | KIASI | MAONI |
|---|---|---|---|
| 1 | Usajili | 20,000 | Kwa Miaka 3-4 |
| 2 | Huduma ya kwanza | 10,000 | Italipwa kila mwaka |
| 3 | Serikali ya wanachuo | 5,000 | Italipwa kila mwaka |
| 4 | Uendeshaji wa mafunzo | 40,000 | Italipwa kila mwaka |
| 5 | Ukarabati | 25,000 | Italipwa kila mwaka |
| 6 | Michezo | 30,000 | Italipwa kila mwaka |
| 7 | Vifaa vya usafi | 20,000 | Italipwa kila mwaka |
|  | **JUMLA** | **150,000** |  |

**N.B:** Ni lazima kwa kila mwanachuo kuja na rimu mbili (02) za karatasi nyeupe na aziwasilishe Ofisi ya masuala ya wanachuo. Rimu mbili hutumika kwa muhula mmoja tu, pia, anaweza kuwasilisha rimu nne (04) kwa mwaka.

## 10.0: VIFAA ANAVYOTAKIWA KUJA NAVYO MWANACHUO

### 10.1: Vifaa vya Malazi na usafi wa mwili

- Blanketi **1.**
- Shuka jozi **2 za rangi ya bluu** na mto wenye **foronya ya** bluu.
- Kandambili
- Ndoo moja ya lita kumi
- Sabuni
- Mswaki na dawa ya meno
- Mafuta ya kupaka mwili

### 10.2: Vifaa vya Michezo

**WASICHANA**

- Jezi moja ya taifa stars ya bluu

- Sketi nyeusi fupi ya kuvaa juu ya suruali
- Track suit ya bluu ya rangi ya bendera Taifa
- Raba nyeupe na soksi zenye ufito kwa juu

**WAVULANA**

- Jezi moja ya taifa stars ya bluu
- Track suit ya bluu ya rangi ya bendera ya Taifa
- Raba nyeupe na soksi zenye ufito kwa juu

**10.3: Vifaa vya Chakula**

- Sahani
- Bakuli
- Kikombe
- Kijiko

**10.4: Vifaa vya Usafi**

- Ufagio mmoja (soft-broom)
- Ufagio mmoja wa chelewa
- Fyekeo moja
- Jembe moja
- Squizer moja
- Reki moja na

**N.B: Hutapokelewa na kusajiliwa kama hujanunua vifaa hivyo vya usafi.**

**10.5: Vifaa vya Masomo**

- Daftari 6 (Counterbook quire four)
- Non-programmable Calculator (Kwa masomo ya Sayansi) yenye function 551-991, mathematical set, penseli, kalamu za bluu au nyeusi
- Vifaa vya Tehama kama vile flash, laptop na smart phone vinaruhusiwa na atahusika kwa ulinzi wa vitu vyake yeye mwenyewe.
- Koti refu na jeupe la maabara kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi

**10.6: Vitabu**

Kila mwanachuo anayesoma masomo ya sayansi anatakiwa kuja na angalau nakala moja ya vitabu vifuatavyo kwa kila somo katika masomo aliyochaguliwa kwa ajili ya kujisomea.

**PHYSICS**

1. Mehta V.K & Mehta R.(2008) *Principals of Physics Class Xi*; S. Chand & Company PVT. Ltd New Delhi India
2. Mehta V.K & Mehta R.(2008) *Principals of Physics Class Xii*; S. Chand & Company PVT. Ltd New Delhi India
3. Nelkon M. & Parker R (2004) *Advanced Level Physics 7th Ed*; Heinemann Educational Books. London
4. TIE (2020) *Advanced Level Physics Form five*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
5. TIE (2020) *Advanced Level Physics Form Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam

**CHEMISTRY**

1. Jain S.K (2008) *Conceptual Chemistry Class Xi*; S. Chan & Company PVT Ltd New Delh India
2. Jain S.K (2008) *Conceptual Chemistry Class Xii*; S. Chan & Company PVT Ltd New Delh India
3. TIE (2020) *Advanced Level General Chemistry Form five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
4. TIE (2020) *Advanced Level Physical Chemistry Form Five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
5. TIE (2020) *Advanced Level Organic Chemistry Form five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
6. TIE (2020) *Advanced Level Inorganic Chemistry Form Five & Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam

**BIOLOGY**

1. Tylor D.J etal (1997) *Biological Science 3rd Ed*; Amazon Publishers, New York
2. TIE (2020) *Advanced Level Biology Form five*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
3. TIE (2020) *Advanced Level Biology Form Six*; Tanzania Institute of Education, Dar es Salaam
4. Toole G. & Toole S. (2014) New Understanding Biology 4th Ed: Oxiford University Press. London United kingdom

**ADVANCED MATHEMATICS**

1. Backhouse J.K & Houldsworth S.P.T (1985). *Pure mathematics 1 3rd Ed*; Longman Publishers. London
2. Backhouse J.K & Houldsworth S.P.T (1985). *Pure mathematics 2 3rd Ed*; Longman Publishers. London
3. Sadler A.J (1967) *Understnding Pure Mathematics*; Oxford University Press, London United Kingdom.

**NB: Mwanachuo ahakikishe anakuja na vitabu vya kiada vya kidato cha tano na sita vya mtaala uliboreshwa 2014 toleo la 2023 kulingana na masomo anayosoma.**

**Mwanachuo wa masafa anapaswa kuwa na vitabu vitakavyomsaidia kujifunza kozi husika atakayodahiliwa. Unaweza kutembelea tovuti ya Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kujisajili katika maktaba mtandao.**

## 11.0 SARE YA CHUO: -

### A. WASICHANA:

- Sketi 2 dark blue zenye rinda moja tu, shati 2 zenye mikono mirefu, shati moja liwe rangi ya light blue na shati jingine rangi nyeupe, na tai 2 ndefu za rangi ya dark blue, Viatu vyeusi vya kutumbukiza visivyo na urembo wowote vyenye visigino vifupi jozi 2 na soksi nyeupe ndefu za kufika juu karibu na goti jozi 2.
- Koti lenye rangi ya dark blue inayofanana na sketi.

  **MUHIMU:** Sketi iwe ndefu hadi usawa wa kifundo cha mguu. Wanachuo wa dini ya kiislam waje na hijab (juba) mbili nyeupe zisizofunika viganja vya mikono pamoja na baibui jeusi kwa ajili ya kwenda kufanya ibada ya ijumaa.

### B. WAVULANA:

- Suruali 2 dark blue zisiwe na marinda, mzunguko wa chini (turnup) na wala zisiwe za kubana (model). Pia, unatakiwa uwe na mkanda mweusi, shati 2 zenye mikono mirefu, shati moja liwe rangi ya light blue na shati jingine rangi nyeupe na tai 2 ndefu rangi dark blue, viatu vyeusi vya kamba jozi 2 na soksi nyeusi jozi 2 pamoja na koti lenye rangi ya dark Blue inayofanana na suruali na lenye mipasuo miwili nyuma.
- **NB:** Sare zote zinatakiwa kuwa na mshono ulioainishwa hapo chini katika picha namba 1 kwa wasichana na namba 2 kwa wavulana. Ikiwa kuna mkanganyiko wa kutambua rangi halisi inashauriwa mwanachuo kushona sare mara afikapo chuoni baada ya kuona rangi halisi inayotakiwa.
- Wanachuo waislamu wanatakiwa wawe na kanzu na kofia nyeupe kwa ajili ya kwenda Ibada ya Ijumaa.

**PICHA Na. 1** **PICHA Na. 2**





**12.0 USAFIRI**

Unatakiwa ujigharamie mwenyewe kwa nauli ya kuja chuoni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.

**13.0 CHAKULA**

Chuo kinatoa chakula kulingana na maelekezo ya serikali. Chuo hakiruhusu wanachuo kujipikia mabwenini au mahali popote katika eneo la chuo. Hivyo mwanachuo haruhusiwi kuja na vifaa vya aina yoyote kwa ajili ya kupikia. Chuo hakina chakula maalum **(special diet)** kwa wanachuo wenye matatizo ya afya.

**NB: Mwanachuo haruhusiwi kuwa na vifaa vya umeme kama pasi, jagi la kuchemshia maji wala kifaa chochote cha kuchemshia ama kupikia, jiko la aina yoyote, kifaa cha umeme cha kukaushia nywele, mshumaa, redio, na silaha ya aina yoyote. Ikiwa mwanachuo atakutwa na vifaa hivi atasitishiwa mafunzo.**

**14.0 MAWASILIANO:**

Mawasiliano yoyote yanayomhusu mwanachuo kutoka kwa ndugu zake au nyumbani **LAZIMA** yapitie kwenye uongozi wa Chuo, kwa Namba zifuatazo:
**Mkuu wa Chuo**: 0752416009
**M/Mkuu wa Chuo**: 0767908900
**Mwadili**: 0754918468

**15.0 NIDHAMU**

Kwa wakati wowote mwanachuo awapo chuoni, anatakiwa kufanya mambo sahihi kwa wakati sahihi, mahali sahihi, na njia iliyo sahihi kwa mujibu wa

maelekezo ya **KANUNI/NGUZO** za chuo ambazo atazipata mara atakapofika Chuoni.

## 16.0 MWISHO

Kila siku unategemewa kuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa kutekeleza **"MOTTO"** wa Chuo ambao ni **"TAA BORA – ANGAZA DAIMA".**

**KARIBU CHUO CHA UALIMU TABORA**

.................................

**Balbina L. Joseph**
**MKUU WA CHUO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU TABORA
S.L.P 320, TABORA

**Nakala:**
Mkurugenzi Msaidizi Mafunzo ya Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P. 10,
**40479 DODOMA.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**TABORA TEACHERS' COLLEGE**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

DATE……………………………………………………………….
Mr/Mrs/Miss…………………………………………………… **(NAME IN FULL)**

Please examine the above named as to **HIS/HER** physical and mental fitness for a full time Teacher Training Course. The Examination should include the following categories.

1 Eye sight
2 Hearing
3 Limbs
4 Speech
5 Veneral deseases
6 Leprosy
7 Epilepsisy
8 Neorosis
9 Other serious deseases
10 Pregnancy

---

## MEDICAL CRTIFICATE

(To be compeleted by Government medical officer)

I have examined the above named and consider that **HE/SHE** is physically **FIT/UNFIT** and mentally **FIT/UNFIT** to full time Teacher Training Course.

1 Eye sight…………………………………………………………………
2 Hearing…………………………………………………………………..
3 Limbs……………………………………………………………………
4 Speech……………………………………………………………………
5 Veneral deseases…………………………………………………………
6 Leprosy…………………………………………………………………..
7 Epilepsisy………………………………………………………………..
8 Neorosis…………………………………………………………………
9 Other serious deseases…………………………………………………
10 Pregnancy……………………………………………………………………

**Approved by :**

**Name………………………………Signature…………………. Date…………………….**